



Australian
BORDER FORCE

Habari muhimu juu ya mipangilio ya karantini ya lazima kwa wasafiri ambao wanasafiri kwenda Australia

Habari muhimu juu ya mipangilio ya karantini ya lazima kwa wasafiri wanaowasili nchini Australia

13 Agosti 2020

Kujibu janga kubwa ya COVID-19, Australia imeweka vizuizi vya kusafiri na matakwa ya karantini ya lazima.

Wasafiri wote wanaowasili nchini Australia wanahitaji kuingia karantini ya lazima ya siku 14 katika mahali pa kwanza pa kufika nchini Australia.

Wasafiri watatolewa na malazi ya kufaa mnamo kipindi hiki na hawatakuwa na ruhusu kusafiri katika nchi (pamoja na makazi ya nyumbani) au kuendelea na maunganisho yoyote ya nchi hadi kipindi cha siku 14 cha karantini ya lazima kimekwisha.

Serikali za majimbo na wilaya, pamoja na kusaidiwa na Serikali ya Australia, husimama mipangilio ya karantini. Katika majimbo mengi na wilaya, utakuwa kuombwa kulipa mchango kwa gharama ya karantini. Habari zaidi inaweza kupatikana kwenye tovuti za kufaa za afya za serikali ya jimbo na wilaya.

Wasafiri wa kupitia

Wasafiri wa kupitia wa kimataifa wanaowasili nchini Australia wanaweza kuondoka na ndege nyingine ya kimataifa ambayo inaondoka kutoka mji ulipofika. Wasafiri wa kupitia wanapaswa

- kuka kwenye kiwanja cha ndege kama unahitaji kungoja kwa ndege nyingine yako, hadi kwa muda wa masaa 8
- nenda kwa karantini ya lazima kwenye kituo cha kuchaguliwa cha jimbo kama muda wa kungojea kwa ndege yako nyingine ni kutoka masaa 8 hadi 72

Wasafiri wa kupitia hawawezi kusafiri katika Australia, hata kupanda ndege ya kimataifa ambayo inaondoka kutoka mji mwingine.

Nini cha kutazamia unapofika nchini Australia

- Utahitaji kufuata maelekezo yote yanayopewa kwako na wafanyakazi wa ndege na maafisa ya serikali wakati unapofika nchini Australia.
- Utapata mzigo wako na utapita michakato ya kawaida ya kibali cha mpaka (forodha, uhamiaji na usalama wa uhai).
- Kufuata kibali cha mpaka, maafisa ya serikali watakuuelekeza kwa basi ambazo zitakuchukua kwa makazi yako.
- Labda utahitaji kusubiri kwa kipindi kiasi hadi kufika kwa makazi yako. Maafisa ya serikali watajitahidi kufanya vipindi vya kusubiri kadiri starehe inavyowezekana. Mashirikiano yako na uvumilivu wako una thamani.

Mipangilio kwa kipindi chako cha karantini cha siku 14

- Maafisa ya serikali kwenye malazi ya karantini watakuwa wanangoja wasili wako. Watafurahi kujibu maswali yoyote unayo baada ya wasili wako na kukusaidia wakati wa kipindi chako cha karantini.
- Malazi hayo yatakuwa na vifaa vyote na huduma zote ambazo utahitaji wakati wa kuka kwako. Malazi yatakuwa pamoja na malazi, chakula, maji ya salama na ya safi, na msaada wa matibabu.
- Ikiwa una mahitaji ya afya, kwa mfano maagizo kwa madawa ya kila mara, mipangilio itafanywa kutekeleza matakwa hayo.
- Unaweza kupimwa kwa COVID-19 katika masaa 48 ya kwanza na ndipo kati ya siku 10 na siku 12 ya karantini. Kama hukataa kupimwa, unaweza kuhitaji kuka karantini kwa kipindi cha kirefu zaidi. Mipangilio sahihi ya kupimwa inategemea majimbo na wilaya.
- Chini ya Sheria ya Usalama wa Uhai 2015 na sheria zinazofaa za jimbo, utahitaji kuka katika malazi yaliyopewa hadi umepata kibali cha kimatibabu ili kuingia jamii ya Australia.

Mipangilio hiyo itakuwa kulazimishwa na serikali za majimbo na wilaya na kusaidiwa na wakala ya Serikali ya Australia.

Kumaliza kipindi chako cha karantini ya siku 14

Punde tu umemaliza kipindi cha karantini ya lazima, unaweza kusafiri katika Australia. Tafadhali ufahamu kuwa majimbo na wilaya yanaweza kuwa na matakwa ya kuingia na ya karantini. Unapaswa kuangalia matakwa ya kuingia na karantini kwa kila jimbo na wilaya kabla kusafiri.



Australian
BORDER FORCE

Habari muhimu juu ya mipangilio ya karantini ya lazima kwa wasafiri ambao wanasafiri kwenda Australia

Tovuti ya Idara ya Afya ya Serikali ya Australia ni pamoja na maungo kwa habari ya majimbo na wilaya juu ya vizuizi vya kusafiri
<https://www.health.gov.au/news/health-alerts/novel-coronavirus-2019-ncov-health-alert/coronavirus-covid-19-restrictions/coronavirus-covid-19-advice-for-international-travellers#quarantine-for-incoming-travellers>